kisichozidi miaka 20 au faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shillingi laki tatu, au vyote kwa pamoja.

### viii. Kuishi kwa Pato la Ukahaba
Ni kosa kwa mwanaume au mwanamke kuishi kwa kutegemea kipato cha ukahaba. Adhabu kwa kuishi kwa pato la ukahaba kifungo kisichozidi miaka 2 au kulipa faini au vyote viwili kwa pamoja.

### ix. Kumiliki Danguro
Ni makosa kwa mtu yeyote ambaye ametenga nyumba, chumba, vyumba au sehemu yoyote kwa nia ya ukahaba. Adhabu ya kosa hilo ni kifungo kisichozidi miaka 2 au kulipa faini au vyote viwili kwa pamoja

### x. Kujaribu Kutoa Mimba
Ni makosa kwa mtu yeyote kujaribu kuharibu mimba kwa kujaribu kumlisha au kumfanya ale sumu au kitu kingine cha kudhuru kwa lengo kuharibu mimba. Adhabu ya kosa hilo ni kifungo cha miaka 14.

### xi. Kuharibu Mimba
Ni makosa kwa Mwanamke kuharibu mimba kwa kula sumu au kitu kingine cha kudhuru au kutumia nguvu ya namna yoyote au akatumia njia yoyote nyingine iwayo kwa lengo la kuharibu mimba. Adhabu ya kosa hilo ni kifungo cha miaka 7.

### xii. Kutoa dawa au vifaa vya kutoa mimba
Ni kosa kwa mtu kutoa dawa au vifaa huku akijua kwamba dawa au kifaa hicho kinakusudiwa kutumika kuharibu mimba. Adhabu ya kosa hilo ni kifungo cha miaka 3.

### xiii. Ulawiti
Mtu atakuwa ametenda kosa la ulawiti katika katika mazingira yafuatayo;

a) Kumuingilia mtu kinyume na maumbile;
b) Kumuingilia mnyama; na
c) Kuruhusu mwanaume kumuingilia kinyume na maumbile;

Adhabu ya kosa la ulawiti inaweza kuhukumiwa kifungo cha maisha au kifungo kisichopungua miaka 30 jela. Hata hivyo ikiwa kosa hilo limetendwa kwa mtoto mwenye umri usiozidi miaka 18 adhabu itakayotolewa ni kifungo cha maisha jela.

Ni kosa pia kwa mtu yeyote ambaye atajaribu kutenda kosa la ulawiti akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka 20.

### xiv. Shambulio la Aibu kwa Mvulana wa chini ya miaka 18
Ni makosa mtu yeyote ambaye atamfanyia shambulio la aibu kijana wa umri wa chini ya miaka 18. Haitakuwa ni utetezi kwa shitaka hilo kuonyesha kwamba mvulana huyo alikubali kutendewa kitendo hicho cha aibu. Adhabu ya kosa hilo ni kifungo cha maisha jela.

### xv. Matendo ya Aibu Baina ya Wanaume
Ni makosa kwa Mwanamume yeyote iwe hadharani au katika faragha kutenda kitendo chochote cha aibu pamoja na mwanaume mwingine au kumfanya mwanaume mwingine kufanya kitendo hicho na yeye. Adhabu ya kosa hilo ni kifungo cha miaka 5.

### xvi. Kuzini na Maharimu
Kosa la kuzini na maharimu hufanyikwa kwa;

a) Mwanaume kufanya ngono na mwanamke ambaye anamjua kuwa ni ndugu yake kama vile mjukuu wake, binti yake, dada yake au mama yake. Adhabu ya kosa hili ikiwa msichana au mwanamke ni chini ya miaka 18 ni kifungo kisichopungua miaka 30 na akiwa na zaidi ya umri wa miaka 18 ni kifungo kisichopungua miaka 20.
b) Mwanamke yeyote mwenye umri wa zaidi ya miaka 18 ambaye anaridhia na kuruhusu ndugu yake kama babu yake, baba yake, kaka yake au mtoto wake wa kiume kujamiiana naye. Adhabu ya kosa inaweza kuwa ni kifungo cha maisha au kifungo kisichopungua miaka 30, mahakama pia inaweza kutoa amri ya kulipa fidia kwa mhanga.

## 2:0 HITIMISHO

Uwepo wa makosa ya kujamiiana au kimaadili katika sheria unalenga kulinda jamii dhidi ya vitendo vyovyote vinavyokiuka maadili na utu wa binadamu na pia kuimarisha na kuboresha staha na heshima ya binadamu wote. Ili kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa sheria jamii ina nafasi kubwa katika kutoa taarifa na ushahidi kwa vyombo vya upelelezi na Mahakama kuhusiana na matukio ya kihalifu yaliyobainika ili haki iweze kutendeka na wahalifu kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria na hivyo kukomesha vitendo hivyo.

---


**Kwa maoni, wasiliana na Tume kupitia anuwani ifuatayo:**

Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,
Jengo la Taaluma Na.1
Barabara ya Mkalama
S.L.P 1718
DODOMA - TANZANIA

tumesheria.tanzania | www.lrct.go.tz
@tumesheria | TumesheriaTv

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



# MAKOSA YA KIMAADILI

# MAKOSA YA KIMAADILI

## 1. 0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Tanzania ilianzishwa mwaka 1980 kupitia Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kufanya tafiti za sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Tume pia inajukumu la kufanya tathmini za utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kubaini kama malengo ya kutungwa kwa sheria hizo yanafikiwa. Tume vilevile ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma ili kuweza kuwajengea wananchi uelewa wa sheria mbalimbali na hivyo kusaidia wananchi kushiriki kikamilifu katika maboresho ya sheria.

## 1. 1 MAKOSA YA KUJAMIIANA

Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura 16 inaainisha makosa ya kujamiiana ambayo ni yafuatayo:

### i. Makosa ya Ubakaji

Makosa ya ubakaji yanafanyika kwa kumwingilia mwanamke na itahesabika kuwa tendo hilo limefanyika iwapo kuna muingiliano hata muingiliano hata kwa kiasi kidogo unatosha kuthibitisha kosa la ubakaji, ushahidi wa kukataa kama vile majeraha yanayoonekana kwenye mwili sio muhimu kuthibitisha kulikuwa na muingiliano.

**Kosa la ubakaji hutendeka kwa kumuingilia mwanamke katika mazingira yafuatayo;**

a). Kumuingilia mwanamke asiye mke wake au mke waliyetengana pasipo ridhaa yake. Hata hivyo ieleweke kuwa wanandoa watachukuliwa kuwa wametengana kama kutengena kwao kunajulikana katika familia au ndugu wa ukoo;

b). Kumuingilia mwanamke asiye mke wake kwa ridhaa yake, pale ambapo ridhaa yake imepatikana kwa kutumia nguvu, vitisho, kwa kumuogopesha au kumtishia kumuua au kumjeruhi;

c). Kumuingilia mwanamke asiye mke wake kwa ridhaa, pale ambapo ridhaa hiyo imetolewa baada ya mwanamke huyo kupewa kilevi cha aina yoyote mfano pombe au madawa ya kulevywa na hivyo kutokuwa katika akili timamu;

d). Ridhaa imetolewa na msichana au mwanamke huyo kwa kufikiri kuwa mwanaume husika ni mume wake na pia mwanaume huyo anajuwa kuwa ridhaa hiyo imetolewa na msichana au mwanamke huyo kwa kuaminishwa kuwa mwanaume huyo ni mume wake;

e). Bila ridhaa yake au kwa ridhaa yake kumuingilia msichana mwenye umri wa chini ya miaka kumi na minane;

f). Mtu kwenye mamlaka ya uongozi ambaye anatumia fursa hiyo ili kulazimisha mahusiano kazini na hivyo kutenda tendo la ubakaji kwa msichana au mwanamke;

g). Kuwa katika nafasi ya uongozi au mfanyakazi katika hospitali, shule, kituo cha uangaliazi cha watoto, nyumba ya watoto, au taasisi nyingine inayofanana na hizo na kutumia nafasi yake hiyo kutenda kosa la kubaka msichana au mwanamke;

h). Kuwa katika nafasi ya uongozi au mfanyakazi anayehusika na mahabusu au sehemu nyingine yeyote ya uangalizi, iliyoanzishwa kisheria au taasisi ya wanawake au watoto na kutumia nafasi yake hiyo kutenda kosa la kumbaka msichana au mwanamke yeyote aliyechini ya uangalizi wake;

i). Kiongozi wa dini kutumia nafasi yake ya uongozi kutenda kosa la kubaka msichana au mwanamke; au

j). Mganga wa kienyeji kutumia nafasi yake hiyo kumuingilia msichana au mwanamke ambaye ni mteja kwa kudai ni sehemu ya tiba.

## ADHABU YA MAKOSA YA UBAKAJI

Adhabu ya kosa la ubakaji ni;

a). Adhabu ya ukomo ni kifungo cha maisha na isiyopungua miaka thelathini (30) pamoja na adhabu ya viboko na faini, na kutakiwa kulipa fidia ya kiasi kitakacho amriwa na Mahakama;

b). Ikiwa kosa limefanyika kwa msichana wa chini ya umri wa miaka 10 atawajibika kwa adhabu ya ukomo ya kifungo cha maisha;

c). Mvulana wa umri wa miaka 18 au pungufu, ataadhibiwa ikiwa-;

(i). Ni mkosaji wa mara ya kwanza, atahukumiwa adhabu ya viboko tu;

(ii). Ni mkosaji wa mara ya pili, atahukumiwa kifungo cha miezi 12 pamoja na adhabu ya viboko; na

(iii). Ni mkosaji kwa mara ya tatu au mhalifu sugu, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka 5 pamoja na adhabu ya viboko.

### ii. Kubaka kwa Kundi

Makosa ya kubaka kwa kundi yanahusisha kumwingilia mwanamke kwa kundi kunakofanywa na zaidi ya mhalifu mmoja. Hivyo kila mshiriki atahesabika kuwa ametenda kosa la kubaka kwa kundi. Adhabu ya kosa la kubaka kwa kundi ni kifungo cha maisha bila kuangalia kiwango cha uhusika wa mhalifu katika ubakaji huo. Ikiwa miongoni mwa washitakiwa hao yuko mshitakiwa mwenye umri chini ya miaka 18 adhabu yake itakuwa ni viboko kulingana na uhusika wake.

### iii. Kujaribu Kubaka

Kujaribu kubaka kunahusisha tendo la mhalifu aliyedhamiria kufanya ubakaji na akashindwa kukamilisha uhalifu aliyodhamiria kuufanya. Kosa la kujaribu kubaka litahesabika ikiwa mtu atatekeleza yafuatayo;

a). Kumtishia msichana au mwanamke kwa lengo la kumuingilia;

b). Mtu mwenye madaraka au ushawishi kwa msichana au mwanamke huyo, kutenda kitendo chochote cha kumtishia ili aweze kumuingilia;

c). Kutoa kauli ya udanganyifu kwa lengo la kupata idhini yake;

Adhabu ya kosa la kujaribu kubaka ni kifungo cha maisha na kisichopungua miaka 10.

### iv. Unyanyasaji wa watoto kingono

Vitengo vifuatavyo dhidi ya mtoto vitahesabikia kuwa ni unyanyasaji wa kingono;

a). Kumruhusu mtoto yeyote kuwa kwenye sehemu yoyote kwa nia ya kufanikisha mtoto huyo kudhalilishwa kijinsia au kushiriki kwa namna yoyote katika matendo ya ngono au maonesho ya ngono;

b). Kufanya ukuwadi kwa mtoto kwa nia ya mtoto huyo aweze kufanya ngono au adhalilishwe kingono au kushiriki katika maonesho ya ngono;

c). Kumshawishi mtu kwa njia ya matangazo yaliyochapishwa au njia nyingine ya habari ili awe mteja wa mtoto katika vitendo vya kingono au aina yeyote ya udhalilishaji wa kijinsia, au maonesho ya ngono;

d). Kumtishia au kutumia nguvu dhidi mtoto, kwa nia ya kumlazimisha mtoto kufanya ngono au kudhalilishwa kingono au kushiriki katika maonesho ya ngono; au

e). Kumpatia mtoto au wazazi wake fedha, vitu au faida nyingine kwa nia ya kumpata mtoto huyo ili afanye ngono au udhalilishaji wa kingono wa namna yoyote au kushiriki katika maonesho ya ngono.

Adhabu ya kosa la unyanyasaji wa watoto kingono ni kifungo ni kisichopungua miaka 5 jela na kisichozidi miaka 20. Mahakama inaweza kuamuru mshitakiwa kumlipa fidia mhanga.

### v. Shambulio la Kingono

Shambulio la Kingono hufanywa kwa nia ya kujitosheleza matamanio ya kimwili kwa kutumia sehemu zake za siri au sehemu yoyote ya mwili wa binadamu au kifaa chochote au tundu lolote au sehemu yoyote ya mtu mwingine pasipo ridhaa yake, katika mazingira ambayo hayahusishi mazingira ya kosa la ubakaji.

Adhabu ya kosa hilo ni kifungo kisichopungua miaka 20 na kisichozidi miaka 30, na pia ataamriwa kulipa fidia ya kiasi kitakachoamuliwa na mahakama kwa mtu yeyote aliyetendewa kosa hilo na maumivu aliyosababishiwa mtu huyo.

### vii. Ukuhadi wa ukahaba

Kosa la ukuhadi wa ukahaba hufanyika katika mazingira yafuatayo;

a). Kumfanya mwanamke au mwanaume wa umri wowote, kwa idhini au bila ya idhini yake kuwa kahaba, ndani ya Jamhuri ya Muungano au nje ya Jamhuri ya Muungano;

b). Kusababisha mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18 au mtu yeyote wa umri wowote kuondoka katika Jamhuri ya Muungano, kwa ridhaa au bila ridhaa yake na kwenda nje ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili shughuli za ukahaba;

c). Kumleta katika Jamhuri ya Muungano mtu yeyote mwenye umri wa chini ya miaka 18 kwa nia ya kumshirikisha kwenye ngono haramu na mtu yeyote hapa ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano;

d). Kusababisha mtu yeyote kwa ridhaa au bila ridhaa ya mtu huyo, kuondoka kwenye maskani yake anayoishi katika Jamhuri ya Muungano kwa nia ya kumhusisha mtu huyo na ukahaba, kuishi au kuhudhuria kwenye danguro, ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano;

e). Anamfungia mtu yeyote bila ridhaa ya mtu huyo kwenye danguro lolote au sehemu yoyote kwa nia ya kufanya ngono haramu au udhalilishaji wa ngono kwa mtu huyo Akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka 10 na